TANGAZO LA SERIKALI Na. 814 la tarehe 10/11/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA BULYAHEKE MBUGANI YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Bulyaheke Mbugani ya mwaka, 2023.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Eneo la Upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa eneo

3. Mipango ya jumla na ya kina kwenye eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa.

*Tangazo la Serikali Na. 814 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Iimetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK1 yenye majira - nukta 422713.289MS, 9746496.267KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa MS72$^0$MS kwa umbali wa kilomita 1.2 kwa kukatisha barabara ya iendayo Kanyala hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK2 yenye majira - nukta 423921.384MS, 9746441.771KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa KS142$^0$MS kwa umbali wa kilomita 1.0 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK3 yenye majira - nukta 424652.935MS, 9745810.573KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS155$^0$MG kwa umbali wa kilomita 0.5 kukatika barabara iendayo Itabagumba hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK4 yenye majira - nukta 424495.937MS, 9745304.040KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa K94$^0$MG kwa umbali wa kilomita 1.1 kukatisha barabara iendayo Kakobe hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK5 yenye majira - nukta 423447.457MS, 9745552.025KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KS170$^0$MG kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MPK6 yenye majira - nukta 422713.289MS, 9746496.267KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ128$^0$MG kwa umbali wa kilomita 0.7 hadi ulipoanzia.

Dodoma,
19 Oktoba , 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*